Mwaka 1871, Stanley aliingia katika Afrika ya Mashariki ili amtafute Livingstone. Watoto, msikose kuwakumbuka sikuzote wazazi wenu na mwalimu wenu pia. Usiseme uwongo. Msizarau mtu ye yote (69). Unipe franka kumi ninunue kitabu kimoja. Kitu hiki hakitumiki : ukitupe. Siwezi, lakini usimwambie mtu. Tusome vitabu vyema na tuvienneze popote. Chui anatafuta mbuzi amle. Msingoje wakati wa mwisho. Unipe bilauri ya maji ninywe. Rafiki yangu, njoo tucheze ! Sherti niende zangu. Nipe

kiti nikae. Unipeleke chakula nisife njaa. Ninakuomba unisaidie. Waacheni watoto waje kwangu, wala musiwazuie. Usi-mwambie mtu mwingine maneno haya. Ningoje mpaka vyote viwe tayari? Ondoka kitandani sasahivi uende kufanya kazi mashambani. Unipe bunduki yako nimwue tai ile akiruka (79) juu ya mti ile. Unipe mshahara wangu, kwa sababu nimefanya kazi kwa bidii. Tusikilize hadisi ya watu wa kwanza waliokaa (85) katika nchi yetu. Mwili wa ndege umefanyiwa waweze kuruka hewani; mwili wa samaki, waweze kuogelea majini. Nenda kwa mwalimu wako, umwombe akupe kitabu kipya kimoja. Mwanamke hukaa nyumbani apike chakula na ashone mavazi ya jamaa yake. Mtu huyu anakaa usiku wote karibu na shamba yake alinde mavuno yake. Tokeni nyumbani, simameni karibu na mlango, mningoje kitambo kidogo. Kama (75) unataka kula matunda, sherti upande katika mti kwa kuyaangusha. Asubui unapoamka (96), imekupasa unawe mwili wako na maji safi. Lazima tutafute mahali pakavu kwa kujengako (90) nyumba yetu. Mganga anafanya juhudi awaponye wagonjwa. Kila kijana anapashwa kufuata mashauri ya wazee. Utupe sisi leo chakula chetu cha kila siku. Mfalme aliamuru watu wote wa makabila yote wahesabiwe (72). Akimwona nyoka (79), mwindaji alitokeza upanga alani amkate kichwa chake. Uwapende watu wote. Uvipende viumbe vyote. Tuliingia mwituni ili tupumzike chini ya miti kitambo kidogo. Hatuna budi tulipe kodi. (Imetupasa tulipe kodi). Lazima mvuvi anunue wavu mpya. Enda masomoni kila siku uwe mtu wa akili. Tuimbe wimbo mzuri tuwafurahishe wazazi wetu. Ninakisoma kitabu hiki kusudi nijue ginsi wanavyoishi (92) watu wa nchi nyingine za dunia. Watu wa kabila letu hawana budi *kuhama* katika nchi nyingine wasife kwa njaa. Nimeweka chumvi katika nyama isioze. Utaweka boma mzingo wa nyumba yako kwa *kuwazuia* wanyama wakali wasiingie. Usimwogope mtu huyu; analia tu; si mbaya hata kidogo. Uwaambie wageni hawa waingie nyumbani mwetu wale chakula nasi. Mpishi anawasha moto apike nyama. Binti anateka maji kisimani asafishe nyumba. Nilimwambia mfalme awape watu wote haki yao.

Exercice XXV

(Fait suite à la leçon XXIX)

Watoto wa mji huu hawana mavazi machafu. Kama (75) unakwenda masomoni, hutakuwa mjinga. Watu wa zamani walikuwa

wajinga. Kesho nitakuwa na koti mpya. Usiwe mvivu : uvivu ni kilema kibaya. Watu wa kwanza walikuwa ama windaji ama wavuvi. Siwe na haya kufanya kazi ya mikono. Usiwe mwongo ; useme ukweli. Kama (75) mtumishi anataka kusafisha nyumba yote (69), kweli hatakuwa na wakati wa kupumzika hata dakika moja. Mwanafunzi ana kitabu chake? — Anacho. Hana. Wanafunzi wana vitabu vyao? Wanavyo. Hawana. Askari wana bunduki zao? Wanazo. Sina kisu, lakini mwenzangu anacho. Hatuna muhogo ; tuende katika jirani wetu ; anao. Palikuwa na mtoto, jina lake Biringa ; alikuwa mdogo kuliko (70) watoto wengine wote. Mlikuwa na maji mengi kisimani. Kutakuwa na watu mengi katika karamu. Hapo kale kulikuwa na tembo katika Ulaya. Kesho kutakuwa na michezo mjini mwetu. Kutokuwa na mali si kilema hata kidogo. Hatuna mkate tena. Maskini huyu hana kitu cha kula. Mwaka kesho nitakuwa na *nafasi* ya kurudi nchini mwangu. Mtu maskini huyu hana kitu, ila (75) mbuzi mdogo mmoja. Sisi, Wakongomani, tunapashwa, hata tuwe wa kabila gani, kutumika kwa *kuistawisha* nchi yetu. Nendeni masomoni kila siku, muwe wanafunzi wema. Vijana wote, wawe wanaume, wala wanawake, wasiotumika (86) ni karibu na *kilema* chochote. Mtoto wangu, uwe mwepesi kwa kusikia, lakini mzito kwa kusema.

Exercice XXVI

(Fait suite au n^o 68 de la leçon XXX)

Mtu mwema, mbaya, mdogo, mkubwa, mwingine. Watu wema, wabaya, wadogo, wakubwa, wengine, wengi, wachache. Mti mrefu, mwema, mzuri, mwekundu, mwingine. Miti mirefu, myema, mizuri, nyekundu, mingine, mingi, michache. Njia pana, nyembamba, ndefu, nyingine, njema, nzuri, mpya. Njia pana (pluriel), nyembamba, ndefu, nyingine, njema, nzuri, mpya, nyingi. Kitabu kipya, kizuri, kibaya, kichafu, chingine, cheupe. Vitabu vipya, vizuri, vibaya, vichafu, vyingine, vichache, vingi. Tawi refu, jeupe, jeusi, jekundu, nene, jingine. Matawi marefu, meupe, meusi, mekundu, manene, mengine, mengi. Uso mzuri, mweupe, mweusi, nyekundu, chafu, nyingine, nyingi. Pahali pazuri, pakavu. Kufa kwema, kubaya.

Mtu maskini huyu hana chakula cha kutosha. Nitakwenda mwaka ujao kukaa katika nchi ya kupendeza. Nyumba safi, ndiyo *sifa* ya mwanamke. Wakati wa mazika maua ya ajabu

yanapamba myitu, pori na bustani. Selemani alikuwa mtu mwenye hekima. Mwana wangu ni mwanafunzi mwenye kufikiri. Watoto wote wanapenda kucheza katika pwani penye mchanga kwa kujengako (90) ngome ndogo na majembe yao mafupi. Mtu mwenye haki hasemi uwongo mara hata moja. Katika pahali penye maji-maji vinaonekana vidudu vya kila namma. Tangu miaka mingi dunia imefanyiwa mabadiliko ya ajabu. Kweli motokaa, ndiyo gari la ajabu. Mjomba wangu ni mtu mwenye nguvu, hata watu wote wanamwogopa. Watu wenye mali mengi wataacha mali yao yote katika saa ya kufa. Ngano inalimwa (72) katika nchi za baridi nusu. Adabu ya watoto ni jambo la lazima. Nilimwona macho mawili katika pango la giza. Mtu huyu hana kazi ya kawaida. Ndugu yangu alihama katika nchi ya mbali. Hekima ya mzee kinatuonyesha kichwa chake chenye *mvi*. Watu wenye mali wanapashwa kusayidia watu maskini wasiwe na njaa. Mimi si razi : hukufanya kazi vema. Bwana wangu amenipa zawadi moja ya samani. Mtu wa haki anaweza kutumaini kuwa na siku moja heri ya milele. Simba mkali alimchinja mwana kondoo. Ninapenda kutembea katika nchi yenye kivuli. Watoto wote wenye umri wa myaka sita wanapashwa kwenda masomoni kila siku. Heri watu wenye njaa na kiu cha haki, kwani *watashiba*. *Wamisri* walikuwa watu wenye dini sana. Angalioni *msimzarau* mmojawapo katika watoto wale.

Exercice XXVII

(Fait suite au n° 69 de la leçon XXX)

Zaruba imeangusha miti yote. Watu wengi wanasahau ya kwa-mba watu wote ni ndugu. Mwalimu, tafazali, unipe kitabu chingine. Kima wamekula matunda yote ya mti huu. Nani ameiba shoka langu? Mimi mwenyewe. Kama (75) unataka kujua siri zote za kiswahili, umepashwa ufanye kazi zote za kitabu hiki chenyewe. Kokote niendako ninapata nafasi ya kumsayidia mmojawapo. Na miti watu wafanya meza, viti, vitanda, mashua, vipini vya majembe na vitu vinginevyo. Ye yote atakaye anaweza kujifunza kusoma. Siku moja mmojawapo wa wanafunzi aliingia masomoni na aliiba kitabu cha mwalimu. Kila mwaka naenda kuwaangalia wazazi wangu wazee mjini mwa kuzaliwa kwangu. Katika Kongo wakaa Baluba, Babemba, Basanga, Bateke, Bakongo na watu wengineo. Katika Kongo kuna wanyama wakukwa : tembo,

faru, viboko na wengineo. Kasuku hawezi kutamka kila lisemwalo, ila maneno machache tu. Hupanda muhindi katika Kongo, Amerika, *Misri* na nchi nyinginezo nyingi. Mwalimu, tafazali, unipe kitabu chochote, buku lolote na kazi yoyote. Katika wanafunzi wa masomo mmojawapo angeweza (83) kuzidi kujifunza; naye atakuwa labda mwalimu. Mfalme aliwapa watumwa wake ruhusa ya kutembea pahali popote walivyotaka (92). Ondoeni vitabu vyote : tumekwisha (99) kusoma. Ninataka kuinunua ngozi ile kwa samani yoyote. Zamani za kale makabila ya Afrika yalipigana (77) yenyewe kwa yenyewe. Wanawake wa mji wetu wanachanganya ugali na kitovero chochote. Lazima mtu ye yote afe kwa kuwaokoa watu wengine wote. Sisi wenyewe tumesikia ngurumo ya simba. Wasafiri *walirejea* kwa njia nyingine. Nita-mfuata rafiki yangu kila aendako. Kila asemalo ni uwongo. Katika mji wetu hakuna hata mmojawapo anaweza kuwaponyesha wakoma, ila mganga mzungu. Uwongo *haufai* neno lolote.

Exercice XXVIII

(Fait suite à la leçon XXXI)

Hakuna kiumbe hodari kuliko simba, ndiyo sababu ameitwa (72) mfalme wa wanyama wote. Afrika ni bara tunapokuta (90) wanyama wakali kuliko wote wa dunia. Nyumba yangu ni nzuri sawa na yako. Mwalimu ni mwema sawa na baba, Nguruwe huyu ni nono kuliko wote. Maji haya ni safi zaidi ya yale. Ua huu ni mzuri kuliko yote. Kosi ni kubwa kuliko kasuku. Urefu wa mtende unapita huo wa mgomba. Chui ni mkali kuliko simba. Mizigo hii ni mizito sana. Nyumba ya sultani ni kubwa kuliko zote. Shaba ni ngumu kuliko chuma. Kazi ya sermala ni nyepesi kuliko kazi ya mehimbaji. Nyumba yetu ni karibu na kanisa kuliko yako. Sultani wetu ni mwema kuliko wenu. Kanzu ya kike ni nzuri zaidi ya kanzu ya kiume. Tembo ni nyama kubwa kuliko wote. Miguu ya nyuma ya sungura ni mirefu kuliko hiyo ya mbele. Matunda haya ni mabivu sawasawa. Nguo ni rahisi hapa kuliko kwetu. Mkono wako wa kushoto ni mehafu; mkono wa kiume ni mehafu zaidi. Simba anapita chui kwa nguvu. Shingo la twiga linashinda hilo la wanyama wo wote kwa urefu. Ingawa (76) nguo hii ina bei kubwa kuliko ile, nitainunua kwa kuwa hodari zaidi. Nguo hii sawa na hiyo kwa uhodari. Mtu huyu ana nguvu ndogo tu.

Exercice XXIX

(Fait suite à la leçon XXXII)

Mwanafunzi huyu anaandika vizuri sana. Kitabu hiki hakinipendezi hata kidogo. Matunda haya hayatoshi kwa watoto wote ; leta zaidi. Kazi yako nzuri kabisa. Mlimaji anaanza kazi yake mapema. Mwana wangu hafanyi kitu masomoni ; anacheza tu. Hima mwivi alitoka nyumbani. Bwana, tunachoka sana ; utupe ruhusa ya kupumzika kitambo kidogo. Ulifanya kazi yake ovyo. Kwa nini umetenda hivi? Sijui vizuri ginsi watu walivyofanya (92) kazi ile. Imekupasa kujaribu vingine. Amekiua kitabu hiki bei gani? Soma polepole : sisikii unayosema (91). Mtu huyu alingoja *marejeo* ya mwana wake, lakini bure. Mna maji haba kisimani. Sababu gani amefanya vile kazi yake? Maua haya yananuka vibaya. Wanafunzi wote wa masomo yetu wanaandika vilevile; wanaandika kama mwalimu wao anavyoandika (92). Twende sokoni pamoja. Andika kazi yako barabara, kama nilivyofundisha (92). Kwa kawaida wanyama wa pori wanakimbia upesi wanapona (96) mtu ye yote. Umekunywa pombe mno : akili yako itapotea. Kuna matunda tele nehini kwetu. Nguo hii, kiasi gani? Hatutaikata miti ile kesho ; watu haba kazini. *Punde kwa punde* mtu yule *anapayapaya* (102) kama *mpumbafu*. Ingieni nyumbani kimya. Mara chui alitoka mwituni. Simchukui mtu aliyenikosea (90), bali ninampenda bado. Fanya kazi hii vivi hivi.

Exercice XXX

(Fait suite à la leçon XXXIII)

Nyumba ya nyuki inaitwa mzinga. Magonjwa mengi yameletwa na vidudu, *kwa mfano* malaria, ugonjwa wa usingizi, homa. Magonjwa mengi yametiwa na uchafu, kwa mfano ukoma na upele. Zamani ya kale watu wa Afrika waliuzwa (97) kama watumwa sokoni mwa pwani. Watu wengi wameuawa vitani. Vijana hawaruhusiwi kuvuta tumbako. Matunda ya mgomba yaitwa ndizi. Watu wabaya wapelekwa mbele ya mwamzi. Mwili wa ndege umeumbwa ili wapate kuruka hewani ; mwili wa samaki umeumbwa ili wapate kuogelea majini. Nyumba za Wazungu zimejengwa ama kwa matofali ama kwa mawe. Nimefundishwa na mwalimu wangu yote niyuayo (91). Binti huyu ataolewa na kijana

wa mji wa karibu. Maziwa ya ngombe yatumiwa kwa kufanya siagi (manteka) na jibini. Madini ya namna nyingi yanapatwa katika Katanga na yanapelekwa katika Ulaya kwa kugeuzwa katika mashini ya ajabu. Vyombo vyote vinavyotumiwa (85) kwa kuwalisha na kuwavalisha watu, kwa kuwajengea (73) nyumba zao, na pia vitu vinginevyo, vimepelekwa katika mji wetu ama na magari ama na wapagazi. Walipokuja (96) watoto masomoni mara ya kwanza, walipewa vitu vyingine, kwa mfano : *kijibao* cha jiwe, kalamu ya jiwe, kitabu cha masomo ; vitu hivi vinatosha muda wa mwaka wa kwanza wa mafundisho. Mwana wangu atapewa jina la mjomba wake. Kijana huyu atamwoa binti wa sultani ; binti huyo ataolewa naye. Ncha ya mlima yafunikwa na wingu la moshi mweusi. Stanley na wenzake walifika katika ziwa linaloitwa (85) Tanganika. Mitumbwi inavutwa kwa *makasia*. Kitabu hiki kimeandikwa ili watu wenye kujua kifaransa wapate kujifunza kiswahili. Nyumba yangu *inazungushiwa* na boma la *michongoma*. Mwanamke huyu *alifiwa* na mumewe wako alipokuwa (96) bado *kijana*. *Msihukumu*, nanyi hamtahukumiwa. Mti huu hupasuliwa mbao. Sultani aliamuru watumwa wakatwe kichwa. Umeuliza na unajibiwa. Chini ya udongo wa shamba langu nimepata vyombo vilivyofinyangwa (85) na watu wa zamani. Bilauri imefanyiwa kwa kioo. Mwezi ujao watu wote watapewa *jozi* moja ya viatu. Watu wote wa mji ule wamepelekwa utumwani na Waarabu. Mwindaji aliingiwa na hofu. Mtu amejibiwa ya kwamba baba yake amekufa tangu miezi miwili. *Usishindwe* na ubaya, bali uushinde ubaya kwa wema. *Washindani* walipokewa na *shangwe*.

Exercice XXXI

(Fait suite à la leçon XXXIV)

Wabeleji wafanya bidii kwa kuwafalia watu wa Kongo. Kwa sababu mwana wangu anajifunza vema, nitamnunulia kitabu kimoja. Mjomba wangu ametufikia juzi. Kesho mama atakwenda sokoni ; atatuletea ndizi na kalanga. Mpagazi amenichukulia mizigo yangu. Umeniambia ya kwamba utakwenda sokoni juma lijalo ; tafazali, unichagulie mbwa mdogo kwa kulinda nyumba yangu. Chui amelikaribia kundi lako la mbuzi. Mama anazipikia *jamaa zake* chakula chenye utamu. Mungu, ninakuomba, unipe neema kushinda tamaa ya mali. Mtumishi amenivunja chombo

kizuri hiki ; nimemkaripia, kwa kuwa kitu hiki kilinipendeza kabisa. Mama, nitakurudushia nini kwa mema wote ulizoniletea(90) tangu kuzaliwa kwangu? Tumwachie mwalimu wetu mlango wazi aweze kuingia masomoni. Rafiki yangu mpenzi, ninakutakia mwaka mwema na mwenye heri. Mtoto mbaya huyu amemwondolea *koo la kuku* vifaranga vyake vyote. Mtumishi, uniletee kikombe kimoja cha kahawa kila asubui. Sasa watu weusi wanajijengea nyumba za matofali, pahali pa misonge ya majani. Watu wale hawana silaha kwa kujilindia. Watoto wema wanamchumia mama yao maua mazuri. Mama amenichagulia nguo nzuri kwa kunishonea kanzu mpya. Baba, unifungulie mlango wa kibanda, ili nipate kutokamo(91). Watoto wabaya wale walitwaa mawe wantupie mbwa. Kwa nini umenitendea vile? Alipofika (96) ndugu yangu, aliniambia habari za mjini mwangu. Simba alinjia anile. Chatu alimkaribia mtu kimya, akamzungusha (81) na nguvu, akamkatia pumzi, hata mtu alikufa. Nikiona (79) mwalimu wangu, ninamjia nimwamkie. Nitamwendea kwake wakati wa usiku. Ndugu yangu ameondoka mjini mwetu tangu miaka mitatu ; nilimwandikia barua sina jibu lolote. Mwamzi *alimwonea* mkosefu *huruma*.

Exercice XXXII

(Fait suite à la leçon XXXV)

Nyoka hana wala miguu kwa kutembea wala mabawa kwa kuruka. Kisha ya masomo watoto wanarudi kwao bila kukawia. Baada ya miaka mitatu Stanley alifika katika pwani ya Bahari Kubwa ya Atlantika. Wasafiri walikaa kitako karibu na chemchem wapumzike. Mwili wa chui unafanana na huo wa paka, kwa maana wanyama wawili wote ni wa jamaa sawa. Kwa sababu gani umekula matunda yote niliyokupa (90) jana? Si tendo jema ; wewe ni mlaji sana ; huna rafiki hata mmoja. Nazani ya kwamba watu wema watapata siku moja tuzo la mwendo wao. Ingawa kuna watu wengi wasiojua (86) kusoma, yafaa kwenda masomoni. Ijapo wazazi wako wamekupa uzima wa mwili, huwezi kusahau ya kwamba mwalimu wako amekupa akili na elimu. Ikiwa hujui kusoma, yafaa uende masomoni. Ikiwa unafanya kazi hutakuwa na njaa hata mara moja. Usiku uliopita niliona baridi kabisa kitandani, ingawa nilifunikwa na blanketi mbili. Ingawa kulima ni kazi ngumu, halali kusema ya kwamba kazi huyo inamletea mlimaji heri

na uhuru. Ijapo unakuja masomoni, hutajifunza kitu, kwa sababu hufanyi kazi yako na *juhudi*. Mlimaji ule hana juhudi kwa kazi : kwa hiyo hatapata mavuno mazuri. Upanga umo ndani ya ala. Tangu lini umepata uhuru? Usumbura ni mji mzuri kando ya ziwa la Tanganika. Umekata mtende ama mchungwa? *Bila shaka* wasafiri watafika bado. Kama unafanya kazi yako ovyo, wewe *utastahili* kuazibishwa. Katika Sahara tunakuta watu waitwao (86) « nomades », yaani watu wasio na (88) makao. Katika Afrika ya Kati, kuna jito moja pana kuliko yote ya bara, yaani Kongo. Jana rafiki yangu alinjia kwa kutembea pamoja mashambani. Kiisha ya miaka mitatu ila siku moja, Stanley pamoja na watu wake walifika katika mlango wa jito Kongo. Hatuoni mtu hata mmoja. Wavuvi hawajarudi (82) bado. Muda wa mwaka mzima watu wa mji wetu wameugua kwa magonjwa mbalimbali.

Exercice XXXIII

(Fait suite à la leçon XXXVI)

Maadui walikuwa karibu kupigana. Mamba na viboko hupatikana hasa katika nchi zenye maji. Hujulikana tembo upesi kwa umbo la kichwa chake, kilicho (87) kinene sana. Yafaa (78) ndugu waandikiane barua. Baba na mama wanapendana kabisa. Mbuzi wawili walikutana katika kilalo chembamba, wakagombana (81), wakapigana, mwisho wakaanguka pamoja mtoni. Kwa kuonana, rafiki yangu mpenzi ; nitarudi kwako bado kidogo. Yafaa watu *wasameheane* makosa yao. Wanafunzi wa masomo yangu wana-shindana kwa kupata tuzo la mwalimu. Nyuma ya vita sherti maadui wapatane kwa kuweka amani kati ya mataifa yao. Stanley na Livingstone waliamkiana, wakazungumuzana (81) muda wa saa nyingi. Jogoo amewika : jua litaonekana bado kidogo. Kwa nini mnagombana? Nyingi si ndugu? Watu waligawanyana *mateka*. Watu wa kabila letu walishindwa katika mapigano, lakini hawakupoteana. Tuache kubishana bure. Chini ya miti ya mwitu wa mvua *kichaka* kimefungamana. Saa ya kufa kwetu haijulikani. Mimi na ndugu yangu tumekutana njiani. Mshtaki na mshtakiwa wamepatana mbele ya mwamzi. Wasafiri walisemeana wao kwa wao : « Tutafanyaje kwa kuuvuka mto mpana huu? Hatuna mtumbwi hata mmoja. » Mimi na mwenzangu tuliachana katika mpaka wa mji.

Exercice XXXIV

(Fait suite à la leçon XXXVII)

Rafiki yako amekudanganya? Haiwezekani! Wakati wa zaruba haifai kujikinga chini ya miti; kuna hatari kubwa kupigwa na radi. Yafaa nikumbuke ya kwamba mwalimu wangu amenipa elimu. Husema ya kwamba watoto wengine hawapendi wazazi wao: haiwezekani! Haramu kutembea katika njia hii. Halali kucheza katika pahali hapa. Siwezi kutoka nyumbani, kwani mvua inakunya sana. Haifai kuwapiga watoto. Siwezi kuona kitu, kwa sababu kuna giza. Kwa kuuvuka mto mpana huu, hatuna budi tutumie mtumbwi imara, kwani mawimbi ni makubwa sana.— Haizuru, nitavuka mto kwa kuogelea. Haifai kutupa njiani maganda ya ndizi. Upindi usio na (88) mishale, wafaa nini? Yafaa tuhame, kwa maana moto umeunguza kibanda chetu. Usitoke nyumbani: mvua inanguruma na inameta. Yapasa tulipe madeni yetu. Kweli, unasoma vizuri. Nitakurudishia feza yako bado kidogo, yakini. Imekupasa uje masomoni. Unapashwa uje masomoni. Ni sherti *ubaguzi* wote kati ya binadamu *ukomeshwe*. Yafaa watu wote waungane. Mtoto wangu mpenzi, haikupasi kuwa wala mwongo, wala mvivu, hata kidogo. Haifai kufuata desturi ya *kishenzi* ya kumwacha bibi na watoto kula jikoni.

Exercice XXXV

(Fait suite à la leçon XXXVIII)

Jioni watu wa mji hukaa kitako karibu na moto, wakihadisia hadisi za kale. Ukitazama samaki akiogelea majini, utaona ya kwamba anafumba na anafumbua kinywa chake. Ukiumwa na nyoka aliye na (88) sumu, imekupasa kuunguza sasahivi kidonda na chuma cha moto. Nikifika mjini nilimwona mtu mzee amesimama mbele ya kibanda chake akivuta kiko. Ukivuma upepo unaangusha miti. Akinguruma usikuni, simba anawaogofya watu wote. Ukitazama mwezi kwa darbini, utaona milima. Mvuvi alimpeleleza samaki akiogelea majini mwa mto. Akijenga nyumba yake katika nchi isiyo (87) kavu, mtu atakuwa na hatari ya kuugua bado kidogo. Akisimama mtoto mgonjwa nyuma ya dirisha la nyumba, alitazama watu wakipita njiani. Watoto walifurahi wakimwona baba ya akirudi nyumbani. Mkila au mkinywa aumkifanya

kitu chochote, fanyeni yote kwa kumheshimu Mungu. Paka hukasirika sana akiona mbwa. Nyoka *ameza* chakula kizima *asikitafune*. Nikifanya kazi, saa zinapita upesi. Nitakusayidia, ukitaka *msaada* wangu. Ngozi yetu itakuwa *nyangavu* zaidi tukitumia maji safi na sabuni kwa kuinawa. Akiingiwa kiboko na *hofu*, *hushambulia* watu. Watu wa pori wanajipatia chakula wakiwinda na wakivua. Nikitembea porini niliona kwa karibu chui akilala katika majani. Akisayidiwa na mke wake, mtu ataweza kumaliza kazi yake mbele ya jioni. Nikipita karibu na kanisa, nilisikia nyimbo nzuri. Ukiyuma na nguvu, upepo unaangusha majani na unavunja matawi ya miti. Wakikaa mahemani, Waarabu wanaweza *kuhamahama* wanapotaka (96). Nikisikia wimbo wa watoto, *nilishangaa* sana. Akitembea njiani, mlevi *alitetereka*. Akiwika jogoo, mji wote unaamka. Ukiwa na mali mengi, usiwasahau watu wasio na (88) kitu. *Adui* yako akiwa na njaa, mlishe; akiwa na kiu, mnyweshe. *Ukisubutu* kuingia nyumbani mwangu, utafukuzwa bila *huruma*. Mume apashwa *kweli* kuwacha babaye na mamaye na *kuambatana* na mkewe, akimpenda kuliko wazazi wake. Ukinililia katika *taabu* yoyote, nitakusikiliza.

Exercice XXXVI

(Fait suite à la leçon XXXIX)

Kuku huyu asipokupa mayayi, nitamkatia kichwa chake. Usipotaka kujifunza masomoni, utakwenda kufanya kazi mashambani. Shamba lisipoharibika na tembo, tutakuwa na mavuno mazuri. Nehi yetu haitaweza kuendelea, yasipojengwa masomo popote. Wasipolima watu mashamba na bidii, hawataweza kutumaini kuwa na mavuno mazuri. Tutakuwa wajinga, tusipokwenda masomoni muda wa utoto wetu. Usiponawa mwili wako kila siku, utapata magonjwa makali ya ngozi, kwa mfano upele ao ukoma. Mfalme aliwakatazia watu wake kurudi mjini, wasiposhinda maadui wa kabila. Asipougua baba yangu, nitakwenda kufanya safari katika Ulaya. Asiponusa mtu ye yote, chui atajongea; tutaweza kumwua na bunduki. Mtumishi atapata mshahara, asipokataa kufanya kasi. Nisipomwua chui, atashambulia kundi la ngombe. Usipofunga mlango wa nyumba, mwivi ataingiamo (90) na ataiba mali yako. Mbuzi atakufa bado kidogo, usipomchinja sasahivi. Usipojua kifransa, sema kiswahili. Nisipokuwa na bunduki, siwezi kumwua simba. Usipolipa madeni yako, utafungwa gerezeni.

Tutashindwa na maadui wetu, tusipopata *msaada* sasahivi. Watu wasipojenga kilalo, hawataweza kuvuka mto. Nisipokuwa na kazi mno, nitakwenda kucheza na mwenzangu. Mikono yako isipokuwa michafu, utaruhusiwa kuandika katika buku. Hutaruhusiwa kumwoa binti yangu, isipokuwa utanipa *mahari* makubwa. Mvuvu hataweza kuvuka mto, isipokuwa atakuwa na mtumbwi imara. Nisipokuwa na kazi, nitasoma kitabu chenye faida. Malaria haiko nchini kusipokuwa mbu. Umeingiaje nyumbani, usipokuwa na kifunguo cha mlango?

Exercice XXXVII

(Fait suite à la leçon XL)

Simba alimwona swala ; akamrukia, akamchinja, akamrarua na kucha zake, akamla. Ibrahimu alisikiliza amri ya Mungu, akatoka mjini mwa kuzaliwa kwake, akahama, akaenda kaskazini, akapigana na maadui zake, akawashinda. Mlimaji alichimba udongo wa shamba, akapanda mbegu, akapalia majani, akangoja wakati wa mavuno, akatuzwa na kazi yake. Mwindaji aliweka mtego. akarudi nyumbani, akaenda mwituni mara nyingine, akaona sungura akikamatwa mtegoni, akamkamata, akamla. Msafiri atatayarisha sanduku yake, akasema « kwa heri », akatoka nyumbani, akapanda katika motokaa, akaondoka sasahivi. Wavuvi waliondoka na nyavu zao, wakaendelea kandokando ya mto, hata wakafika katika pahali penye maporomoko palipo samaki wakubwa wengi. Nyoka alimkamata jogoo, akammeza, akamla, akashiba, akapumzika. Aliposikia (96) mwindaji simba akakaribia, alijificha nyuma ya mti, akaegemeza bunduki begani, akangoja kitambo kidogo, akitazama upande wa pahali aliposikia ngurumo ya nyama. Askari wote waliacha mapigano, wakakimbia, wakarudi mjini mwao, wakiingizwa na haya. Msimamizi alitoka nyumbani, akapanda frasi wake, akaondoka mbio kwa kumkamata mwivikitoroka. Mwenyeji aligawanya shamba lake katika sehemu tano, akampa kila mtu sehemu kwa kupandako mboga. Mzungu yuko wapi? Yuko shambani. Enda, kamwite. Njoo hapa, kanipe bunduki yangu. Ondosha vijiko, kazilete nyuma. Tulipata jangwani maiti mengi ya watu waliokufa (85) kwa kiu, tukayazika sasahivi na heshima. Twaa kalamu na buku na vitabu, ukaende masomoni. Hapo *pazia* la *hekalu* lilipasuka vipande viwili toka juu mpaka chini ; na nchi ikatetemka, na mawe yakapasuka,

na *makaburi* yakafunika. Simama ukaende. Kitendawili kizuri kimoja cha Afrika ; nimeingia mwituni, nikawaamkia *wazima*, hawakuniitikia ; nikawaamkia *wafu*, wakaniitikia. (Jibu : majani mabishi, majani makavu). Watu wengi wanahama mashamba, wakaenda kuishi mjini kwa ajili ya kazi yao.

Exercice XXXVIII

(Fait suite à la leçon XLI)

Baba yetu hajarudi : mfungulie mlango, ili aweze kuingia nyumbani. Mfanya biashara hajapata gari kwa kupeleka biza ya yake. Sijamaliza kazi yangu. Mtumishi wangu hajalipa deni lake. Mwindaji ameumwa na nyoka ; kidonda chake hakijapona. Nimepatana kwa *mshahara* mtumishi mpya ; hajaja leo ; ninaogopa asije. Ndizi hazijaiva : hatuwezi kuzila bado. Hata kabla hawajaja masomoni, watoto walimkutana na mwalimu mara kwa mara mjini ; hawao-gopi kwenda chuoni. Ninamngojea mwenzangu tangu saa moja karibu na chuoni kwa kwenda kucheza naye : hajafika. Mwana-mume wangu mdogo hajaenda masomoni kwa maana ana miaka mitatu tu. Usimwuze ndama kabla hajazaliwa. Watu wengi wa nchi yetu wanakuwa hawajaona (97) kwa karibu mashua ya hewa. Wanafunzi hawajaanza kazi yao, kwa sababu hawajapata kalamu zao. Hatujui barabara jinsi watu wa kwanza wanavyoishi (89), kwani hawajajua kuandika. Mtu huyu hajaoa mke. Sijamwona ngombe wako mzuri umemnunua jana. Sijamwona rafiki yangu kwa miaka mingi (97), labda amekufa katika nchi ya mbali. Kabla nijatwaa bunduki, chui alikuwa amechinja (97) mbuzi mawili. Gari la moshi halijafika bado. Wazazi wangu wameishi miaka mingi sijawa bado. Kabla mama hajaniita asubui, nimeamka tangu saa moja. Sijaona mtu hodari sawa huyu. Sijaenda mbali alipofika (96) mwenzangu. Mama yangu hajapata bado miaka selasini. Sherti ndege ajenge tundu lake kabla ya masika hayajaanza. Umemwona ndugu yangu? Sijamwona. Usikate kanzu kabla mtoto hajazaliwa.

Exercice XXXIX

(Fait suite à la leçon XLII)

Kama ungejua kusoma, ungepata kitabu kizuri. Kama usingepata chakula sasahivi, usingeweza kufanya kazi. Chui angefika,

ningekimbia *kwa haraka*. Ninge kwenda sokoni, ningenunua nyama na samaki. Ningesikia ngurumo ya simba, ningegopa sana. Kama mgonjwa asingepata dawa, angekufa bado kidogo. Ningepajua mahali anapokaa (90) rafiki yangu, ningekwenda kupita siku moja kwake. Ungejaribu, ungepata kuukata mti huu. Usingekuwa na bunduki, usingeweza kumwua chui. Kama ungalifanya kazi jana, ungalipata feza kwa kununua chakula. Mlimaji asingalinunua jembe jipya, asingaliweza kuzidi kazi yake shambani mwake. Ungalikwenda masomoni, ungalijua kusoma. Usingalikuwa na tamaa mbaya, ungaliheshimwa na watu wote. Usingalituletea mkate, tungalikufa kwa njaa. Kama mbuzi wasingalitoka zizini, wasingalichingwa na chui. Ungekuja, ningeondoka. Usingalisema uwongo, ningalikuamini. Ninge kuwa na karatasi, ningekuandikia barua moja. Ningalikwenda masomoni wakati wa utoto wangu, ningejua kusoma leo. Ungaliweka chandarua dirishani, vidudu visingaliingia chumbani. Usingejua kusoma, enda masomoni ili mwalimu akufundishie siri ya *harfu*.

Exercice XL

(Fait suite à la leçon XLIII)

Nijapomaliza kazi yangu ya hesabu, siwezi kwenda kucheza na wenzangu, kwa sababu imenipasa kumsayidia mama yangu. Ajapoandika mtoto mdogo huyu katika buku lake na wino nyeusi, vidole vyake ni safi kabisa. Ujapovuma uepo na nguvu, miti ya shamba langu haikuanguka. Ajapopona baba yangu, hawezi kufanya kazi bado, kwa sababu anachoka sana. Wajapopigana na uhodari, watu wetu wameshindwa na adui. Ijapo wapagazi walikuwa wamechoka (97) sana kwa safari, hawakukataa kwenda mbali zaidi, kwa sababu walikuwa *wakitumaini* (97) kupata mshahara wao. Msizarau mtu ye yote, ajapokuwa maskini, kwa kuwa watu wote ni wana wa Mungu. Kirongozi amewaacha wasafiri njiani, japo alikuwa amepewa (97) feza tele. Wakila ngombe porini, analala usingizi mchungu mvivu, japo simba anazungukazunguka karibu karibu. Japo mchwa ni viumbe vidogo wanaweza kujenga visugulu vikubwa. Nijapokisahau kitabu changu nyumbani, nitakwenda masomoni. Paka huweza kuona ijapokuwa ni usiku. Usizarau adui yake ajapokuwa mzaiifu.

Exercice XLI

(Fait suite à la leçon XLIV)

Ndimi niliyeandika barua hii. Nimeuza nguruwe watatu walio-kuwa wanono kabisa. Mchungaji anawachunga ngombe wanaokula majani ya pori. Mwindaji anampeleleza chui anayezunguka karibu na zizi. Jangwa lililo kubwa kuliko yote ya dunia, ndilo Sahara, lienealo toka Mangaribi mpaka Mashariki ya bara ya Afrika. Wasafiri walifika karibu na ziwa Moero palipo mpaka wa Katanga na Zambia. Lazima mtu anayeendesha motokaa awe na utartibu. Mtu afanyaye kazi yake kwa juhudi anastahili kuheshimwa na watu wote. Nani aliyevitupa vitabu hivi? Kazi inayofanyiwa na mshoni, ndiyo kushona mavazi. Katika nchi zile zilizo karibu na maziwa, hupatikana mamba na viboko. Motokaa ndiyo gari liendeshwalo kwa nguvu ya « benzine », yaani mafuta ya mawe. Mwanamke anajejua kuhesabu hawezi *kupunjwa* sokoni. Karibu na mito yote wapo watu wanaovua samaki. Baba yetu uliye mbinguni. Mtu mmojawapo atakayekataa kwenda kufanya kazi shambani ataazibishwa bila huruma. Ibrahimu alikuwa na mwanamume aitwaye Isahak. Nyumba zilizojengwa katika pahali pa majimaji ndizo asili ya magonjwa mengi. Asiyepanda havuni. Jinsi baba alivyoamuru, ndivyo nifanyavyo. Hakuna *nabii* mmoja aheshimaye katika nchi yake. Atakayeishi ataona. Wasafiri walifika pahali paitwapo Chilatembo. Mtu anayesema uwongo ni mtu wa kuzarauliwa. Mwisho wa maisha yangu, ninatumaini kurudi nchini kwangu nilimotoka. Kilimanjaro ni mlima ulioko katika Tanzania. Jangwa ni nchi isiyo na maji : kwa hiyo haiwezekani kupandako mimea wala kufugako ngombe. Kila aliyepo hapa atafanya kazi. Sijui aliko. Nimempa mtu maskini huyu mavazi yaliyo bora sana. Ndiyo mtu niliyempa sadaka. Ndimi mtu aliyekupelekea jana barua ya baba yako. Mbwa alifuata *nyayo* hata alifika pahali alipo sungura. Tembo anao mkia ulio mfupi sana. *Alaaniwe anayemzarau* baba au mama yake ! Asiyetaka kufanya kazi asile. Ninafurahi sana kwa sikukuu zijazo. Sio watu wazima waliotaka mganga, ila walio hawawezi.

Exercice XLII

(Fait suite à la leçon XLV)

Fuko anakaa katika tundu analolichimba (alichimbalo) chini ya udongo. Mwanafunzi mwema hayasahau *maarifa* aliyoyajifunza

(aya jifunzayo) alipokwenda (96) masomoni. Tufanye yote mwalimu aliyotumuru. Mungu wangu, nitakushukuru milele kwa uzima nilioupewa kwa wema wako. Hili ni pango alipojificha simba tumtafutaye tangu jana. Nyayo alizoziona mwindaji karibu na zizi, ndizo hizo za chui. Sitaki kuliuza shamba nililonunua mwaka jana. Aksanti sana, Bwana, kwa kitabu kile ulichonipa. Kila mtu apenda nehi azaliwako. Kitabu hiki kinatusimulia yote wafanyayo wenzake wa Stanley muda wa safari yao kubwa katika mwitu wa mvua. Mwana wangu amepasua vitabu vyote alivyo navyo. *Mwashi* ataziba nyufa zilizo katika kuta za nyumba. Wasafiri walifika katika pahali pasipo maji. Mpishi anapika chakula changu kama alivyosema. Fanya upendavyo. Utasamehe makosa yetu kama tunavyosamehe waliotukosea. Zamani, kama mjuavyo, watu wa Kongo hawakujua kusoma. Ninafahamu jinsi baba yangu alivyofanya kwa kupata mavuno mazuri. Uwape maskini sadaka kadiri uwezavyo. Fanya yote ninayoambia. Kitu akipendacho zaidi mlimaji, ndiyo mashamba yake. Nitatenda vilevile kama alivyotenda babangu. Kwa nini unataka kuviona vitu vyote nilivyo navyo? Wasafiri walifika katika pahali pasipokuwa na miti. Ndiyo nyumba ya sultani : watumishi wake peke yao wana ruhusa ya kuingiamo. Kitabu ulicho nacho wewe ni kizuri sana. Nataka kutenda sikuzote kama Mungu apendavyo. Barua hii uliyoniletea jana imeandikwa na baba yangu mzee anayekaa Ulaya. Chupani humu, lililo tupu leo, mlikuwamo jana divai nyekundu. Fanya yote atakayokuambia mwalimu. Mtumishi hana haki ya kufanya apendavyo. Usimwambie mtu mambo uliyoyaona na kusikia. Si kama nitakavyo mimi, ila utakavyo wewe. Nilicho nacho ndicho nakupacho. *Wavulana* na *wasichana* wajitayarisha kwa maisha yajayo watakayojichagulia. Maadui waliingia mjini na waliwaua watu wote waliomo. Sijui usemavyo. Umleavyo mtoto wako, ndivyo akuavyo. Uwape maskini *sadaka* kadiri ya *mali* uliyo nayo. Kazi uliyo nayo haitoshi. Rudieni kwenu mtokako !

Exercice XLIII

(Fait suite à la leçon XLVI)

Sumu yenye hatari inajaza kifuko karibu na meno ya nyoka. Nyoka nyingine *wanapofusha* watu wakiwatupia mate ya sumu. Watoto wangu wapenzi, nitawajulisha hadisi ya Stanley, aliyevumbua nchi yetu. Nimetoka nyumbani kimya nisimwamshe rafiki

yangu aliyelala usingizi chumbani mwa karibu. Mafundisho yame-tengenezwa kwa kuwawezesha watoto kuwa watu wa akili. Nikipita katika mji, nilisimamisha motokaa, nikashuka, nikaenda kuwaa-mkia wazee na wagonjwa. Nyimbo zilizonipendeza zaidi, ndizo hizo zinazonisimulia hadisi za nchi yetu. Nikiya masomoni nimepo-teza kalamu yangu njiani. Nitafanyaje? Nitamwomba mwalimu anipe nyingine. Akifika katika Kongo, Stanley aliona mambo *yaliyomhuzunisha*, kwa mfano biashara ya watumwa. Maadui walilazimishwa kukimbia na *haraka*, kwa sababu wameshindwa katika mapigano. Majumba ya mji mikubwa ya Ulaya yana-pendeza machoni sana. Elimu ya Wazungu inawashangaza sana watu wa nchi yetu. Kwa kuwapendeza wazazi wangu, ninajifunza na bidii masomoni. Mchungaji, uwarudishe ngombe zizini, kwa maana ninaogopa chui awe karibu. Mnionyeshe mikono yenu ili niweze kuona ya kwamba ni safi. Uvivu wa wanafunzi unamkasiri-sha mwalimu. Unirudishie feza niliyokukopesha mwaka jana. Nimkumbusha rafiki yangu *ahadi* yake. Kufika kwa rafiki yetu kunawasha moyoni mwetu utumaini wa kuokowa kwa hatari bado kidogo. Ukivuma upepo unayainamisha matawi ya miti. Kama unaongoza gari, usinywe pombe. Kama unakunywa pombe., usiongoze gari. Mchungaji amelipitisha kundi lake la ngombe njiani kwenie miiba. Mbona umetuhamisha katika nchi hii kavu, ili tufe kwa kiu?

Exercice XLIV

(Fait suite à la leçon XLVII)

Ulimi wa nyoka umegawanyika katika ncha mbili. Kwa kitambo kidogo mwendo wa motokaa *uliongezeka* hata kupita kilometro mia katika saa moja. Haifai kujifunza kwa tamaa ya kutajirika tu. Katika mwitu wa mvua na karibu na maziwa kuna vidudu vingi visivyohesabika. Watu wote wa mji walikusanyika, waka-fanya shauri kusudi kuwajengea watoto chuo kipya, Muda mrefu sana vyombo vya mawe na vya mifupa vimetumika, badala ya vyombo vya chuma, tunavyovitumia sasa kwa kurahisisha kazi yetu. Wakati wa *tauni* watu waliteseka sana. Kazi ya watu wa kale ilifanyika kwa mikono tu. Jirani yangu ametajirika upesi mno. Mwili wa mtu umegawanyika katika sehemu nne, ndizo : kichwa, kiwiliwili, mikono na miguu. Wapagazi wamechoka sana ; tuta-wapa ruhusa ya kupumzika muda wa siku mbili. Karibu na ziwa

kulikuwa na vidudu vingi bila kuhesabika. Chokaa inayochanganyika na mchanga inatumika kwa kuunga matofali na vile kwa kujenga kuta za nyumba. Usiku mgonjwa aliamka mara nyingi, kwa kuwa aliteseka sana. Walimaji wanahuzunika, kwa maana mavuno yote yameharibika zaidi na zaidi. Katika nchi ya Waislamu wanawake *wanafunika* uso wao kwa *shela*. Rafiki yangu *alihuzunika* sana kuiacha nyumba yangu. Mlango wa gereza ulifunguka mwenyewe. Bwana, mapenzi yake yafanyike ! Hapana mtu *aliyekamilika*. Wakati wa masika njia hii haipitiki.

Exercice XLV

(Fait suite à la leçon XLVIII)

Akiogelea samaki katika maji, anafumba na anafumbua midomo yake bila kuacha. Watu wenye elimu wa Ulaya wanachimba udongo na wanafungua makaburi waone jinsi watu walivyoishi zamani. Ninapokwenda (96) kulala kitandani, ninafunga macho yangu mara. Asubui anapowika (96) jogoo, ninafumbua macho yangu. Funga kinywa : unasema uwongo tu. Jana nilitega mtego chini ya mti ; tembo akipita leo ameutegua. Nitawezaje kumkamata chui? Haiwezekani. Funua mfuko wako : nazani ya kwamba umeniibia. Mfanya biashara anakunjua nguo kwa kuimwonyesha *mnunuzi*. Kunja nguo hii kaiweke kashani. Watoto, inameni kichwa na inueni mikono. Jioni ninapovua (96) mbele ya kulala, ninaona baridi sana ; *ninafanya haraka* kuvaa shati yangu na kuingia kitandani. Naziba chupa na kizibo ; nalizibua na kizibuo. Watoto wangu wapenzi, mzibue masikio yenu.

Exercice XLVI

(Fait suite à la leçon XLIX)

Wanapomwona simba wanyama wote wanakimbia mbio. Kazi yao ilipokwisha, wachimbaji walikwenda kulala katika kivuli cha miti kwa kupumzika. Watu wote wapenda nchi walipozaliwa. Nilipomwona baba yangu akirudi kwangu, nilifurahi sana, nikamtayarishia chakula chema. Utakapofika kwetu, tutapokewa na furaha kubwa kwa mikono miwili. Nilipoegemeza bunduki begani, ndege zote walikimbia mbali. Wakati alipofika Stanley katika Afrika, watu weusi wengi walikuwa wakiteswa sana na Waarabu.

Waliporudi mjini kiisha ya safari kubwa, wasafiri walinawa na wajiweka tayari kwa kujibu *maswali* ya ndugu zao. Unapotaka kuingia katika nyumba yoyote, usimame kitambo kidogo mbele ya mlango ; *ukagonge* mlango polepole na kidole, ukisema « Hodi » kwa *sauti* wazi ; ukangoje kimya mpaka mwenyeji wa nyumba atakuruhusia kuingia akikujibia « Karibu ». Aliporudi baba yetu, tulimsimulia jinsi tulivyofanya kazi yetu alipokuwa (84) mbali. Watu weusi walikuwa hawajaona kinga walipofika kwao Wazungu wa kwanza. Walipoondoka baba yangu, nililia, kwa sababu niliogopa asirudie tena. Walipofika Wabeleji katika nchi yetu, watumwa wote waliandikwa huru. Alipowashinda Stanley Waarabu, utumwa *ulikoma* kabisa katika Kongo. Nilipopata habari ya kwamba baba yangu aliugua, nilikwenda sasahivi kumwita mganga aje kumwugua. Siku kumi zilizotimia, msafiri alirudi mjini. Mvuvi alipofika kati ya mto, mamba alimwendea ili *azamisha* mtumbwi wake. *Kulipopambazuka*, waaskari wote walitoka mwituni. Ilipokuwa jioni, chui aliingia zizini. *Ilipotimia saa tatu*, mawaziri walikubaliwa kuingia jumbani mwa mfalme. Anapopumzika sungura, masikio yake yameinama.

Exercice XLVII

(Fait suite à la leçon L)

Mtoto alikuwa akisikiliza hadisi babu alikuwa akiyomsimulia. Palikuwa na watoto watatu waliokuwa wakicheza njiani. Watu wote walikuwa wakitembea pamoja njiani mwa mwitu. Watu wa zamani walikuwa hawana mavazi yo yote. Tulikuwa tumezoea kutembea mashambani tukitazama maua na tukisikiliza wimbo wa ndege. Alipokufa baba yangu nilikuwa nimekwisha soma. Nili-poingia masomoni, mwalimu alikuwa akiandika ubaoni. Mwivi amefungwa gerezani kwa sababu alikuwa ameiba feza. Alipofika mwalimu masomoni, wanafunzi walikuwa wakicheza kiwanjani. Mwalimu alikuwa akisimama mbele ya wanafunzi akiwaelezea hadisi ya nchi yao. Sasa tunakwisha vumbua asili ya magonjwa mengi yaliyowatesa watu wa zamani. Rafiki yangu, wewe uliyekuwa umejifunza vitu vingi ukienda masomoni, utaweza kujibu maswali yangu. Sasa tumekwisha soma hadisi ya safari ya Bwana Stanley. Wanafunzi wadogo wa darasa ya kwanza wamekwisha soma kitabu cha pili. *Furushi* uliyokuwa umenipelekea ijafika bado. Wakati wa nilipokuwa nikimngojea mwenzangu karibu na

kanisa, nilisikia kengele ikiwaita watu katika sala. Wakisikia ngurumo ya simba karibu na pahali walikuwa wakikaapo, watu walikuwa *wakitetemeka* kwa *woga*. Wakati wa kale watu wa kaskazini waliacha nchi yao, wakahama kusini, wakafika katika Afrika ya Kati, wakawafuguza *wakazi*, wakajikalia karibu na maziwa makubwa ya Mashariki. Wakati wa kufa, mfalme aliwaita washauri wake karibu na kitanda chake, akawapa amri zake za mwisho, akafumba macho, akazimia. Mti uliokwisha kuanguka kule ndio mtende. Rafiki yangu alikuwa amekwisha fika kwangu. Mwandikaji amekwisha andika barua. Wakati Stanley alipovumbua Afrika ya Kati, mfalme Leopoldo wa pili alikuwa akitawala Ubejeji. Watu wa kwanza walikuwa wakitumia *magogo* ya miti, walipotaka kuvuka mito. Zamani za kale watu walikuwa wakia-budu jua, mwezi, nyota na wanyama.

Exercice XLVIII

(Fait suite à la leçon LI)

Nitamwua simba asijekaribia kundi la ngombe. Lisijekuchwa jua, tutakuwa tumesimika hema. Tunawe mikono yetu asijefika mwalimu. Tumalize kazi yetu asijerudi baba. Usijenunua kinga ulipe kwanza madeni yako. Kila asubui ninaamka asijeniita mama yangu. Lisijeondoka gari, weka mafuta katika magurudumu. Nisijekwenda kulala kitandani, unilete bilauri ya maji baridi. Tusijeimba wimbo mzuri huu aliotufundishia mwalimu wetu, tumalize kwanza kazi yetu ya hesabu. Nisijeandika barua, lazima niende kununua kalamu na wino. Asijekufa simba mzee, alijaribu bado kumchinja mbuzi aliyemwona karibu na chemchem. Asijekata mti, mtu amelinoa shoka lake. Wasijepiga *mzinga*, askari wanaziba masikio yao. Msijeingia masomoni, amkieni mwalimu na heshima. Nitatandika meza barazani, asijefika bwana yangu. Simeon alifumbuliwa kama hatakufa asijemwona Kristu.

Exercice XLIX

(Fait suite à la leçon LII)

Silaha za kizamani zilikuwa mishale na mikuki na mashoka; leo hutumia bunduki na mizinga. Watoto wanaume wapenda kucheza kiaskari. Nimefasiria hadisi hii kwa kiswahili. Watoto,

kaeni kitako kimya. Unajua kusema kifransa? Ninasema kidogo tu. Tazameni kijuujuu : mtamwona tai akiruka juu ya mwitu. Jirani yangu amejenga nyumba yake kifalme. Kisha ya mapigano maadui amekimbia kifujofujo. Nyumbani mwangu ndugu yangu anakaa kikwake. Hattutaki kufuata mazoezo yote ya kigeni. Mti huu umeota kigugu. Wapagazi walikula kiwimawima. *Ngiri* wape-nda kukaa kikundi. Watu wa nehi hii wanalima mashamba yao kikale. Watu hawapendi kuacha desturi ya kikwao. Lugha ya kikwetu, ndiyo kiswahili. Mtoto ana *kikwikwi* : umpe bilauri ya maji baridi kwa *kumtuliza*. Jirani yangu amejenga nyumba ya kishamba. Mume na mke wale wanakaa kindoa. Unasema kiwazimu. Kwa kawaida makarani wanavaa kizungu. Akimwona mtumishi wake kutofanya kitu, bwana alikasirika kimoyo.

Exercice L

(Fait suite à la leçon LIII)

Tukifika mjini, tulisikia vigelegele vya furaha. Alipoondoka paka, panya wanachezacheza nyumbani. Majengo mengi makubwakubwa ya zamani yamejengwa na watumwa. Makabila mengi yanatangatanga katika jangwa. Katika bustani yetu kuna maua ya namna rangirangi. Watu wabaya wanalala kimachomacho tu. Kipepeo ataga mayayi madogomadogo. Watoto walikuwa wakitupatupa mawe madogo huku na huko. Kamba ya furushi inakatikatika. Akitembea kiwete anaangukaanguka sikuzote. Tokeni nyumbani polepole, wazazi wenu wasiwasikie. Vidudu vingi vinarukaruka chumbani ; uvifukuze kwanza ; halafu ukiweke chandarua dirishani. Nyota zametameta mbinguni. *Kimetemete* cha nyota kinafurahisha macho. Akiona matendo mabaya ya watu wake, mfalme alikasirika kimoyomoyo. Mwana wako hawezi kujifunza kusoma, lakini hastahili kuazibishwa, kwa sababu anademadema. Ndizi hizi ni teketeke kabisa ; yafaa kuzila sasahivi. Mama yangu ni tepetepe kwa ugonjwa. Mehawi amewatiatia watu wasifanye kazi. Haifai kujenga nyumba katika pahali majimaji. Akipigwa na jiwe, jitu alianguka kitanitani. Haramu kuacha matakataka karibu na milango. Mtu yule ni wa kigeugeu : nani angeweza kumwamini? Maji yanapita kifulifulu. Wanawake waliwashangalia washindaji na kigelegele cha furaha. Sungura analala usingizi kimachomacho. Kimbelembele ! Kindanindani alizani ya kwamba mtu yule amesema uwongo. Nyoka anameza chakula chake kingu-

vunguvu. Mshindani alianguka kiusouso. Watu wa nehi ile wana-
waya waya porini. Akitumika pa paa ya nyumba, mwashi alianguka
kwa kizunguzungu. Tembo alikanyagakanyaga maiti ya chui kwa
miguu yake. Kwa ulimu wake mbwa alambalamba maji ya mto
na damu ya wanyama. Mbwa hutembeatembea pua yake chini
kwa kuzitafuta nyayo za *mawindo* yake.

Exercice LI

(Fait suite au n° 103 de la leçon LIII)

Kama ungali unasikiliza vema makelele ya usiku, utatambua
kilio cha chui akizunguka katika mwitu apate chakula chake.
Ijapokuwa mwana wangu angali mtoto mdogo bado, anajua
kusoma vema. Jirani yangu angali akiimba tangu asubui hata
jioni. Mlikuwa angali kulala usingizi, alipokwenda zake baba yenu
kwa kuanza kazi yake mashambani. Aliporudi baba nyumbani,
mama alikuwa angali kushona. Ungali bado kijana. Katika nehi
nyingi za dunia, watu wangali kuona njaa. Majengo makubwa
ya zamani yaliyojengwa kwa mawe, yaangali bado kushinda
mashambulio ya wakati hata sasa. Wageni wanaosafiri katika
Kongo wanasema ya kwamba twangali *tukistawi* kwa ajabu.
Hadisi za watu wa zamani zingali zimesimuliwa katika nehi zote
za Afrika. Ninatumaini baba yako angali mzima. Nazani mpishi
angali sokoni. Mtoto ameamka? — Angali akilala.

Exercice LII

(Fait suite au n° 104 de la leçon LIV)

Sitaka kumwza kuku huyu ambaye ananipa yayi moja kila
siku. Wanafunzi ambao wanajifunza vema wanapata tuzo la
mwalimu wao. Watu ambao wanaungamana pamoja wanafanya
mambo makuu kuliko watu ambao wanafanya kazi peke yao.
Hiki ni kitabu ambacho ndani yake tunasoma hadisi ya *shujaa*
mmoja, jina lake Stanley. Mtu yule ndiye mwalimu ambaye kazi
yake ni kuwafundisha watoto wa mji wetu. Majani ambayo
yamekauka yataanguka chini bado kidogo. Kitabu ambacho nina-
kisoma sasa kimechapwa katika Ulaya. Bunduki hii ambao na
yake nimemwua simba huyu nimeinunua Ulaya mwaka uliopita.
Ndio mshale ambao na yake nimemwua chui mkali ambaye ame-

haribu kundi langu la mbuzi mwezi jana. « Maison » ni neno la kifransa, ambalo maana yake ni « nyumba ». Nitayauza kesho matunda ambayo niliyanunua jana. Katika Katanga kuna madini ambayo hayapatikani pengine. Soko, ndiyo pahali ambako watu wanunua na wauza biza ya. Bandari ni pahali kando ya bahari ambapo zinafika na zinaondoka merikebu za nchi zote za dunia. Ninajua hadisi ambayo nazani itakupendeza sana. Tumepita jangwani ambako maji hayapatikani. Wasafari walitembea nchini ambako chakula hakipatikani.

Nous demandons à nos lecteurs de ne pas nous reprocher d'avoir donné, à certaines phrases du texte français, une forme manquant parfois d'élégance. Nous avons voulu rapprocher le plus possible la traduction française du texte swahili : nous espérons faciliter ainsi l'acquisition des tournures syntaxiques propres aux langues agglutinantes.

TRADUCTION DES EXERCICES

Exercice I

Le bon médecin, le médecin blanc, le rusé pêcheur, le pauvre vieillard, le robuste cultivateur, les apôtres du Christ, le disciple de Mahomet, l'Arabe *de Zanzibar*, le petit-fils du vieil homme, les bons domestiques de l'Européen, les compagnons du porteur, les pâtres du roi, le mauvais sorcier, les mauvais sorciers, les hommes noirs d'Afrique, les hommes blancs d'Europe, les hommes rouges d'Amérique.

Le bon cuisinier aide la femme. Le secrétaire écrit la lettre. L'enfant lit le livre. Le porteur porte des charges. Le malade crie. Le terrassier creuse la terre. Pierre et André étaient des disciples de Jésus. Le chef (de caravane) conduit la caravane. Les porteurs *marchent à la file* dans la forêt. Le terrassier emploie la houe. Le porteur *porte sur le dos* une charge trop lourde. Le roi de notre région est un homme très méchant. Le roi de votre région n'est pas un homme méchant. Trois enfants jouent. Deux hommes arrivent. Trois femmes cousent des habits. L'enfant, l'instituteur, le médecin, le domestique et le cultivateur sont cinq hommes (personnes). Le bon cuisinier cuit la nourriture. Les hommes du village *dansent*. Les chasseurs et les pêcheurs sont des hommes rusés. Les ivrognes et les voleurs sont des hommes mauvais. Le roi a beaucoup d'esclaves. Les hommes noirs habitent en Afrique, les hommes blancs habitent en Europe, les hommes rouges habitent en Amérique. Trois porteurs et deux pâtres, c'est combien d'hommes?

Exercice II

La main sale, les mains sales, le bras long, le grand bananier, les beaux maniocs, la scie affilée, les lourdes charges, les petits clous, le salaire du domestique, les méchantes flèches des sauvages, les beaux arbres de la forêt, l'extrémité de la rivière, le parapluie noir de la femme, le début de l'année, la fin du mois, les trois lourdes charges des porteurs, les deux pièges du chasseur, les nombreuses épines de l'arbre, l'autre jeu des enfants, la fumée noire du *volcan*, les courtes racines du maïs, le corps de l'homme.

Le commencement de tout travail est difficile, la fin est facile. Les racines de cet arbre sont longues et grosses. La marche des voyageurs est très pénible. Ferme cette porte-ci, ouvre cette porte-là. Le grand arbre tombe. Le domestique a cassé trois jarres. L'arbre de la forêt a des épines méchantes. La flèche de l'homme se casse. Mon père peut porter des charges très lourdes. Les domestiques coupent de grands arbres. Les charges des porteurs sont trop lourdes. Le corps du lézard ressemble au corps du crocodile. Les os des oiseaux sont très légers. Les palmiers sont de très grands arbres. Trois pirogues traversent la large rivière. Une épine de l'arbre blessa la main de l'enfant. Le parapluie protège de la pluie. Demain les chasseurs reviendront au village. Ce jeu amuse les enfants du village. J'aime Dieu de tout mon cœur. Une année a douze mois. La queue de l'éléphant est très courte. L'homme travaille avec les mains, il marche avec les jambes. Mes parents ont bon cœur. Le rusé chasseur prit le léopard au piège. Les mains de cet enfant sont très sales. Le carré a quatre côtés. Jésus-Christ est mort en croix.

Exercice III

La bonne nourriture de l'homme, la hutte sale de l'esclave, la grosse tête de l'éléphant, les hautes montagnes d'Afrique, les beaux livres de l'instituteur, un tourbillon de fumée, les trois parties du corps, les cinq doigts de la main, la grosse bosse, les passions de l'ivrogne, le gué facile de la rivière. l'ombre agréable du bananier, plusieurs créatures de Dieu, les deux souliers de l'enfant, les oiselets de l'arbre, le ponceau du ruisseau, la dignité du roi, la clef de la porte, les petits sièges de la chambre.

